بَرَكَةُ الرِّضَا

BARAKA KWA SABABU YA KURIDHIKA

Amesema Hasan Al-Baswriy (Allaah amrehemu):

«مَنْ رَضِيَ بِمَا قَسَمَ اللَّهُ لَهُ، وَسِعَهُ وَبَارَكَ اللَّهُ لَهُ فِيهِ، وَمَنْ لَمْ يَرْضَ لَمْ يَسَعْهُ وَلَمْ يُبَارَكْ لَهُ فِيهِ»

“Atakaeridhika na kile ambacho Allaah amemgawia, kitamtosheleza, na Allaah atamtilia baraka ndani yake, na asiyeridhika hakitamtosheleza wala hatobarikiwa ndani yake”[1]

Mwandishi
Sheikh Ahmad Bin Mubaarak Al-Mazrui *** **Mfasiri**
Abu Halima Arafat

[1]- Ameipokea Ibn Abi Ddun-ya katika kitabu: [Ar-Ridhwaa ‘anillaahi waqadarih] (Uk. 112).

Katika Athari hii kuna faida nyingi na pia kuna tahadhari:

Faida ya Kwanza: Allaah ndiye anayegawa riziki za waja, yeye ndiye humpa amtakaye na humnyima amtakaye, na humzidishia riziki anayemtaka na humpunguzia anayemtaka.

Amesema Allaah Ta'alaa:

﴿أَهُمْ يَقْسِمُونَ رَحْمَتَ رَبِّكَ نَحْنُ قَسَمْنَا بَيْنَهُم مَّعِيشَتَهُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا﴾

"Kwani wao ndio wanaogawa rehma za Mola wako Mlezi? Sisi tumewagawanyia baina yao maisha yao katika uhai wa duniani"[2].

Kwa hiyo jambo hilo lipo mikononi mwa Allaah, Mjuzi wa yaliyofichika na hakimu muadilifu.

Faida ya Pili: Wajibu wa mja ni kunyenyekea kwenye Qadar (kitu alichopangiwa) na Allaah, na kuridhika kwenye kile ambacho Allaah amemgawia, kwa sababu kuridhika katika mgawo wa Allaah kunamfanya mtu atosheke na kile alichopewa hata kama atakuwa ni muhitaji, na pia Allaah humtilia baraka ndani yake, na pia akiridhia katika majanga na mitihani mbalimbali inayomsibu, Allaah humfanyia wepesi na kumridhia.

Amesema Mtume -Swalla Llaahu alaihi Wasallam-

«فَمَنْ رَضِيَ فَلَهُ الرِّضَا، وَمَنْ سَخِطَ فَلَهُ السُّخْطُ»

"Atakaeridhia atastahiki kupata yeye radhi (za Allaah), na atakaechukia na atastahiki yeye kupata machukivu (ya Allaah)[3].

Kuridhia ni daraja ya juu zaidi kuliko subra, kwa sababu kuridhia kunaleta furaha katika nafsi ya mtu na ukunjufu wa kifua chake.

2- Surat Az-Zukhruf/32.

3- Tirmidh (2397) na Ibn Majah (4031).

Faida ya Tatu: Hatafikia mtu daraja hii ya kuridhia isipokuwa kwa kujua mlango wa Al-Asmaa was-Swifaat (kujua majina ya Allaah na sifa zake), kwa sababu kutamfanya mtu kutanguliza mapenzi ya Allaah, Qadar yake na amri yake ya kilimwengu aliyoipitisha[4], na kwamba tayari ilitangulia katika elimu ya Allaah kujua hekima yake, na kwamba Allaah hakumpatia mtihani huo isipokuwa kuna hekima kubwa ndani yake.

Amesema Imam Ibnul Qayyim **-Allaah amrehemu-** "Mitihani ina hekima nyingi zaidi ya thelathini, na mtu kujua hekima hizi kunamfanya yeye kufikia katika daraja ya kuridhika; (fahamu kwamba):

1. Allaah hakukupa wewe mtihani isipokuwa anataka kukutengeneza wewe, kukurubisha (kwake) na kunyanyua daraja yako.
2. Kupewa mtihani hapa duniani ni katika sababu za kupata nafuu akhera.
3. Pindi Allaah akimpa mja wake mtihani humpa jambo la maumivu.

Na mengine yasiyo kuwa hayo, mambo ambayo humfanya mtu afanye subra na aridhie, kisha ujue kwamba ufalme wote ni wake, na wewe ni mtumwa tu katika dunia hii, na angalia upande mwingine wa kwamba hii dunia ni kitu duni katika pande zake zote, isipokuwa (mtu) kumtii Allaah Subhaanah, na wala hakuna ndani yake ukamilifu wa mwanadamu, kwa hiyo ukiitazama dunia kwa mtazamo huu, na ukaitazama nyumba ya akhera (pepo) na yaliyomo ndani yake mambo yenye ukamilifu, kujitosheleza, na uzuri, basi utajisalimisha na utaridhika[5].

Faida Ya Nne: kuridhika ndio pepo ya hapa duniani, hajui ladha yake isipokuwa yule aliyeonja, na pia kuridhika ndio mahali pa kustarehe nafsi ya mja na kutulizana kwa moyo, na izingatie kauli ya Allaah Subhaanah:

---

[4]- Kwa kuitakidi mtu kwamba hili ni jambo ambalo Allaah alitaka litokee kwangu hapa duniani.
[5]- Tazama kitabu: [Twariiqul Hijratayn] (Jz. 1, Uk. 362).

﴿مَآ أَصَابَ مِن مُّصِيبَةٍ إِلَّا بِإِذۡنِ ٱللَّهِۗ وَمَن يُؤۡمِنۢ بِٱللَّهِ يَهۡدِ قَلۡبَهُۥۚ وَٱللَّهُ بِكُلِّ شَيۡءٍ عَلِيمٞ﴾

“Hautamsibu mtu msiba wowote ila kwa idhini ya Allaah, na mwenye kumuamini Allaah atauongoza Allaah moyo wake, na Allaah kwa kila kitu ni mjuzi”[6].

Aya hii imekutolea wewe mukhtasari wa milango ya mitihani/majanga na jinsi ya kuwa na subra nayo, na (imekuashiria) matunda gani yanayopatikana katika hiyo subra, na njia ipi ya kufikia kwenye huko kuridhia.

Amesema Imam Ibn Kathir **-Allaah amrehemu-:**

"أَيْ: وَمَنْ أَصَابَتْهُ مُصِيبَةٌ فَعَلِمَ أَنَّهَا بِقَضَاءِ اللَّهِ وَقَدَرِهِ، فَصَبَرَ وَاحْتَسَبَ وَاسْتَسْلَمَ لِقَضَاءِ اللَّهِ، هَدَى اللَّهُ قَلْبَهُ، وعَوَّضه عَمَّا فَاتَهُ مِنَ الدُّنْيَا هُدى فِي قَلْبِهِ، وَيَقِينًا صَادِقًا، وَقَدْ يُخْلِفُ عَلَيْهِ مَا كَانَ أَخَذَ مِنْهُ، أَوْ خَيْرًا مِنْهُ".

[Yeyote anayefikwa na msiba na akajua kwamba ni kwa sababu ya hukumu ya Allaah na makadirio yake (amepitisha hivyo), basi akasubiri, na akataraji malipo kutoka kwa Allaah, na akasalimu amri kwa Allaah, Allaah huuongoza moyo wake, na atamfidia kwa yale aliyoyakosa katika dunia (kwa kumpa) uwongofu moyoni mwake, na yakini ya kweli, na huenda akarudishiwa kile kilichochukuliwa kutoka kwake, au bora zaidi kuliko hicho][7].

Jumatatu 25/Jumaadal Uulaa/1444H – 20/12/2022M,

Markaz sheikhil Islaam Ibn Taymiyyah,

Pongwe Tanga.

Simu: 0715-263 253

6- Surat At-Taghaabun/11.

7- Tazama kitabu: [Tafsiiru Ibn Ibn Kathir] (Jz. 8, Uk. 137).